TANGAZO LA SERIKALI NA. 886 la tarehe 15/12/2023

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetenegenzwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa za Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa au afisa yeyote aliyeteuliwa

kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni ni eneo au soko liliotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kama soko;

Sura ya 167

"hifadhi ya barabara" maana yake ni kama iliyoainishwa katika Sheria ya Barabara;

"stendi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"ushuru" maana yake ni maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri husika.

Utozaji wa ada na ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa

6.-(1) Muda wa kukusanya ada na ushuru utakuwa ni

kukusanya ada na ushuru

kuanzia Saa kumi na Mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa katika aya ndogo ya (1).

(3) Malipo ya ada na ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada na ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ukusanyaji wa madeni

7.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu au taasisi itakuwa imeshindwa kulipa ada na ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyoainishwa katika aya ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za wadaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika aya ndogo ya (3) na (4), Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

Uteuzi wa wakala

8.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya Mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Maeneo ya machinjio

9. Mtu yeyote anayetaka au atakayetaka kuchinja mnyama au wanyama atatakiwa kuchinja mnyama au wanyama wake kwenye machinjio yatakayoainishwa na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

10. Bila kuathiri masharti yaliyoainishwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri baada ya muda wa kazi kuisha kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Minara ya Mawasiliano

11.-(1) Mtu yeyote anayetaka kujenga mnara wa mawasiliano atatakiwa kuomba kibali cha maandishi kutoka Halmashauri.

(2) Endapo mtu atajenga mnara wa mawasiliano bila kibali, Halmashauri itatoa notisi ya siku saba ya kuondoa

mnara huo.

(3) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (2), mtu atatakiwa kuondoa mnara huo kwa gharama zake binafsi, na endapo atashindwa kuondoa mnara huo Halmashauri itauondoa na atatakiwa kuilipa Halmashauri gharama zilizotumika.

Makosa na adhabu

12.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii; au

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti yoyote ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

13. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha Shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

### SEHEMU I: USHURU WA MAZAO

| Namba | Aina ya Zao | Kipimo | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mahindi | Gunia | 3,000/= |
| 2. | Maharage | Gunia | 3,000/= |
| 3. | Ndizi | Mkungu | 300/= |
| 4. | Viazi mviringo | Gunia | 3,000/= |
| 5. | Karanga | Gunia | 4,560/= |
| 6. | Ulezi | Gunia | 4,560/= |
| 7. | Muhogo | Gunia | 3,000/= |
| 8. | Viazi vitamu | Gunia | 3,000/= |
| 9. | Njegere | Gunia | 4,560/= |
| 10. | Magimbi | Gunia | 3,000/= |
| 11. | Nyanya | Tenga | 2,000/= |
| 12. | Vitunguu | Gunia | 3,000/= |
| 13. | Parachichi | Gunia | 3,000/= |
| 14 | Matango | Gunia | 2,500/= |
| 15. | Tikitimaji | Gunia | 2,000/= |
| 16. | Alizeti | Gunia | 3,000/= |
| 17. | Mpunga | Gunia | 3,000/= |
| 18. | Tangawizi | Gunia | 3,000/= |

### SEHEMU YA II: USHURU WA MAEGESHO NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

(a) Ushuru wa kuegesha magari kituo kikuu cha mabasi

| Na. | Aina ya Chombo cha Usafiri | Muda | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| (i) | Mabasi makubwa | kwa kila Safari | 5,000/= |
| (ii) | Mabasi ya Kati | kwa kila Safari | 4,000/= |
| (iii) | Mabasi madogo | kwa kila Safari | 2,000/= |
| (iv) | Teksi | kwa Siku | 2,000/= |

(b) Ushuru wa usajili wa Teksi

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Muda | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| (i) | Teksi | Kwa Mwaka | 100,000/= |

(b) Ushuru wa Magari maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Muda | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| (i) | Gari ndogo za kawaida | kwa siku | 1,000/= |
| (ii) | Gari (kuanzia tani $1^1/_2$ hadi $6^1/_2$ | kwa siku | 1,500/= |
| (iii) | Ushuru wa lori (Tani 7) | kwa siku | 2,000/= |
| (iv) | Ushuru wa magari (zaidi ya tani 7) | kwa siku | 2,500/= |

## SEHEMU YA III: USHURU WA MAZAO YA MISITU

| Na. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa kupasua mbao kwa misitu ya Serikali | 5% ya bei ya ubao |
| 2. | Ushuru wa kupasua mbao kwa mtu binafsi | 1,000 kila ubao |
| 3. | Gunia la mkaa | 3,000/- gunia |
| 4. | Mauzo ya nguzo za miti (chini ya sm 20) | 15,000/-kwa kila nguzo |
| 5. | Asali | 200/- kila lita |
| 6. | Nta | 200/- kila lita |
| 7. | Kuni (Sm 1) | 20,000/-kwa tani moja |
| 8. | Ubao futi 7 | 400/-kila ubao |
| 9. | Ubao futi 12 | 400/-kila ubao |
| 10. | Ushuru wa magogo ya kupandwa | 1,000/- kwa kila gogo |
| 11. | Ushuru wa magogo ya asili | 1,000/- kwa kila gogo |
| 12. | Kibali kukata miti ya asili | 65,000/- kwa kila kibali |
| 13. | Usajili mlolongo msumeno kwa mwaka | 100,000/- |
| 14. | Ushuru wa mirunda | 400/- kila mrunda |

## SEHEMU YA IV: USHURU MBALIMBALI WA MIFUGO ADA NA USHURU WA MACHINJIO

(A) Ushuru wa kuchinja

| Na. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2,000/- kwa kila mmoja |
| 2. | Mbuzi au Kondoo | 1,000/- kwa kila mmoja |
| 3. | Nguruwe | 1,000/- kwa kila mmoja |

(B) Ushuru wa Mnada

*Tangazo la Serikali Na. 886 (Linaendelea)*

| Na. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa biashara ya mifugo mnadani<br>Ngómbe au punda | 5,000/= kwa kila Ng'ombe au Punda |
| | Mbuzi au Kondoo | 1,500/= kwa kila mbuzi au kondoo |
| 2. | Ushuru wa malisho au machunga | 2,000/= kwa ngómbe kwa Mwaka |
| 3. | Ushuru wa uzalishaji ngozi ya ngómbe | 1,000/= kwa kila ngozi |
| 4. | Ushuru wa uzalishaji ngozi ya mbuzi au kondoo | 500 kwa kila ngozi |
| 5. | Ushuru wa usafirishaji Ngozi | 10,000 kwa kila kibali |
| 6. | Leseni ya biashara ya mifugo na mazao yake | 105,000/= kwa mwaka |
| 7. | Ushuru wa kusafirisha mbolea ya samadi | 1,000 kwa gari |

## SEHEMU YA V: ADA ZA SHUGHULI ZA BURUDANI NA TIBA MBADALA

### (A) SHUGHULI ZA BURUDANI

| Na. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Disko za siku za kawaida, sikukuu na mwisho wa juma | 20,000/- kwa siku |
| 2. | Waganga wa jadi | 150,000/- kwa mwaka |
| 3. | Michezo ya sanaa za maonesho ngoma au maigizo au sarakasi au michezo ya nguvu. | Shilingi 20,000/- kwa siku katika kumbi. |
| 4. | Shughuli za sanaa za ufundi (uchoraji) picha, upakaji rangi, vinyago | 10,000/- kwa onesho |
| 5. | Kibali cha kuendesha ligi ya mpira wa miguu (kama uwanja haufungwi na kutolewa viingilio) | 50,000/- kwa ligi nzima. |
| 6. | Kibali cha kuendesha ligi ya mpira wa miguu (kama uwanja unafungwa na kutolewa viingilio) | 200,000/- kwa ligi nzima |
| 7. | Kibali cha kuendesha bonanza la Michezo | 20,000/- kwa bonanza zima |
| 8. | Ada ya usajili wa vilabu na vyama vya michezo | 25% ya malipo ya BMT |
| 9. | Ada ya usajili na vibali vya wasanii au Wapiga mziki au Washereheshaji au vikundi vya sanaa za maonesho au kwaya na kumbi za starehe na maonesho | 25% ya malipo ya BASATA |
| 10. | Kunasa kanda za sauti kwa vikundi wakati wa mashindano ama shughuli iliyoandaliwa na Halmashauri | 10,000/- kwa siku |

*Tangazo la Serikali Na. 886 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11. | Kutangaza biashara kwa vipaza sauti | | 20,000/- kwa siku |
| 12. | Vikundi vya sanaa za ufundi | | 10,000/= kwa mwaka |
| 13. | Kuendesha promotion au matangazo katika baa au hoteli au maeneo ya wazi | | 20,000/- kwa siku |
| 14. | Wasambazaji wa cable za runinga (TV) | | 30,000/- kwa mwezi |
| 15. | Kucheza meza za pool | | 10,000/- kwa mwezi |
| 16. | Utundikaji wa matangazo ya vitambaa kwenye barabara | | 2,000/- kwa mwezi |
| 17. | Utundikaji wa matangazo ya karatasi | | 10,000/- kwa mwezi |
| 18. | Sehemu za makumbusho au za kihistoria kwa mtu mmoja: | | |
| | i. | Mtu mzima raia | 1,000 |
| | ii. | Mtu mzima asiye raia | Dola za Kimarekani 10 |
| | iii. | Mwanafunzi wa nje ya nchi | Dola za Kimarekani 5 |
| | iv. | Mwanafunzi wa ndani ya nchi | Bure |
| 19. | Kuendesha utafiti wa mambo ya kale na tafiti nyingine zinazofanana na hizo kwa miezi mitatu: | | |
| | i. | Raia wa Tanzania | 50,000/= |
| | ii. | Asiye raia wa Tanzania | Dola za Kimarekani 70 |

(B) DAWA ZA ASILI NA TIBA MBADALA

| Na. | Aina ya Huduma | Ada (Shilingi) | |
|---|---|---|---|
| | | Mwaka | Siku |
| i | Kuuza madawa ya Tiba Asili kwenye gulio | | 1,500.00/= |
| ii | Kuuza madawa ya Tiba Mbadala kwenye gulio | | 2,000.00/= |
| iii | Kuuza madawa kwa mtoa huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala ambaye amesajiliwa nje ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa | | 3,000.00/= |
| iv | Mtoa huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala ambaye sio Mtanzania | | Dola za Kimarekani 3.0 |
| v | Mtoa huduma za Ukunga | | 50,000.00/= |
| vi | Muuza dawa za Tiba Asili na Tiba Mbadala kwa njia ya Duka au Stoo | | 50,000.00/= |
| vii | Kituo cha Zahanati cha Tiba Asili na Tiba Mbadala | | 100,000.00/= |
| viii | Kituo cha Afya cha Tiba Asili na Tiba Mbadala | | 300,000.00/= |
| ix | Hospitali ya Tiba Asili na Tiba Mbadala | | 500,000.00/= |
| x | Kiwanda cha Kutengeneza dawa za Tiba Asili na Tiba Mbadala | | 150,000.00/= |
| xi | Ukaguzi:<br>Duka, Stoo, Mganga na Mkunga | | 30,000.00/= |
| | Zahanati, Kituo cha Afya Hospitali na | | 100,000.00/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Kiwanda | | |

SEHEMU VI: ADAYA VIBALI VYA UJENZI

(A) VIBALI VYA UJENZI

| Na. | Ukubwa wa eneo | Kiwango cha tozo (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | 46.5$m^2$ | 20,000/= |
| 2 | 46.5$m^2$ hadi 92.01$m^2$ | 25,000/= |
| 3 | 92.01$m^2$ hadi 139.35$m^2$ | 35,000/= |
| 4 | 139.35$m^2$ hadi 185.81$m^2$ | 45,000/= |
| 5 | 185.81$m^2$ hadi 278.71$m^2$ | 60,000/= |
| 6 | 278.71$m^2$ hadi 371.61$m^2$ | 90,000/= |
| 7 | 371.61$m^2$ hadi 464.51$m^2$ | 120,000/= |
| 8 | 464.51$m^2$ hadi 557.42$m^2$ | 150,000/= |

(B) VIBALI VYA KUJENGA UZIO WA KUDUMU

| Na. | Ukubwa wa eneo | Kiwango cha tozo (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | 100.$m^2$ hadi 600$m^2$ | 30,000/= |
| 2 | 601$m^2$ hadi 1600$m^2$ | 50,000/= |
| 3 | 1601$m^2$ hadi 4000$m^2$ | 75,000/= |
| 4 | 4001$m^2$ hadi 6000$m^2$ | 100,000/= |
| 5 | Zaidi ya 6001m2 | 120,000/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 13)*

HATI YA UFILILISHAJI WA MAKOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ya mwaka, 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

*Tangazo la Serikali Na. 886 (Linaendelea)*

MBELE YANGU:
Jina: ……………………………………..……………………
Saini………………………..…………………………..………
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe………………………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Kerywa imegongwa kwenye sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Halmshauri ya Wilaya ya Kyerwa uliofanyika Tarehe …. Mwezi… Mwaka…. na Kushudiwa na Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya :-

SACF. JAMES MARCO
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa*

MH. BAHATI HENERICO
*Mwenyekiti*

*Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa*

NAKUBALI,

Dodoma,
20 Novemba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*